

## MAKTABA YA SHERIA NA KITUO CHA KUTOA MAELEZO

Mahakama kuu ina Maktaba ya Sheria na Kituo cha Kutoa Maelezo kwa bure na wazi kwa umma kwenye ghorofa ya 2 ya korti. Hapa unaweza:

- Pata fomu za kisheria
- Tumia kompyuta na printa
- Fanya fotokopi
- Pata usaidizi wa kupata wakili wa bure na wa gharama nafuu
- Pata huduma zinazopatikana kwa jamii

Wafanyikazi wa Maktaba wanaweza kufikiwa kwa simu

**(520)724-8456**

au barua pepe

[lawlibrary@sc.pima.gov](mailto:lawlibrary@sc.pima.gov)

## AMRI ZA KULINDA NA AGIZO DHIDI YA UNYANYASAJI

Ikiwa wewe au mwanafamilia yako ako katika hatari ya kuwa mhasiriwa wa unyanyasaji wa nyumbani na mtu mwingine wa familia, mume/ mke, au mume/mke wa zamani, au mahusiano mengine, unaweza kuomba Amri ya Ulinzi. Agizo dhidi ya unyanyasaji zinaweza kutumika kwa mizozo kati ya majirani au wageni.

Fomu za Amri ya ulinzi zinahitaji kujazwa kwenye mtandao kwa AZPOINT (<https://azpoint.azcourts.gov>).

## Kabla ya kuomba Amri ya Ulinzi

Unaweza kuzungumza na mtezi wa wathiriwa kabla ya kufaili kwa kupiga simu **(602) 279-2900** au **(800) 782-6400**

Lazima uende kwa korti ya Arizona kuwasilisha ombi lako. Ikiwa jaji atakubali ombi lako, Amri ya Ulinzi itatolewa siku hiyo hiyo. Hakuna gharama ya huduma.

**Ikiwa unahitaji msaada wa lugha kukamilisha fomu za korti, pamoja na Amri ya Ulinzi, wasiliana na CITS (Huduma za korti za Kutafsiri)**

kwa simu  
**(520) 724-3888**

au barua pepe

[sccits@sc.pima.gov](mailto:sccits@sc.pima.gov)

## MALALAMIKO

Ikiwa unaamini hujapewa msaada mzuri wa lugha kwa korti au kesi inayoendelea kwa jaribio, au huduma yoyote inayotolewa na korti, tafadhali wasilisha **Fomu ya Malalamiko kwa Huduma ya Upatikanaji wa Lugha Mahakamani**.

Unaweza kupata fomu hii kwa kupiga simu kwa CITS kwa nambari zilizo juu au kupakua fomu kutoka kwa tovuti ya Mahakama ([www.sc.pima.gov](http://www.sc.pima.gov)).



# SWAHILI

**MWONGOZO WA KORTI  
KWA MTUMIAJI ALIYE  
NA USTADI MDOGO WA  
KIINGEREZA  
(LEP)**



110 W. Congress Street  
Tucson, AZ 85701

**(520) 724-4200**

[www.sc.pima.gov](http://www.sc.pima.gov)

## HUDUMA ZA KORTI ZA KUTAFSIRI (CITS)

**Mahakama Kuu:**  
**(520)724-3888**

Huduma za korti za Kutafsiri (CITS) Idara ya Mahakama Kuu ya Arizona katika Kaunti ya Pima imejitolea kuhakikisha ufikiaji wa maana na kulinda haki za watumiaji wote wa korti. **Ujuzi mdogo wa lugha ya Kiingereza au ulemavu wa mawasiliano havipaswi kuwa vyikwazo kwa kupata haki.**

Ikiwa unahitaji huduma za kutafsiriwa au nafasi maalum kwa kuendesha kesi yako, tafadhali wasiliana na ofisi ya CITS kupanga mkalimani wa lugha inayofaa kabla ya kwenda kortini.

## UNAPOTUMIA MKALIMANI WA KORTI

Unapozungumza kortini, elekeza mawazo yako na maneno yako kwa hakimu au kwa mtu ambaye unazungumza naye (sio Mkalimani).

Mkalimani atakusaidia kuwasiliana na wakili wako, wafanyikazi wa korti, na jaji wakati kesi yako inaendelea.

Kazi ya mkalimani ni kusema haswa kile kinachosemwa, bila kuongeza, kuondoa, au kubadilisha sehemu yoyote ya mawasiliano.

Tafadhali usiulize mkalimani ushauri wa kisheria. Wakalimani hawawezi kuegemea upande wowote kwa sababu za kimaadili

## UNAPOTUMIA MKALIMANI WA MAHAKAMA KUPITIA SIMU

Mkalimani atajitambulisha mwanzoni kabla ya kesi usikilizwa. Ikiwa huwezi kusikia au kuelewa mkalimani tafadhali mjulishe hakimu mara moja, hata ikiwa lazima ukatize usikilizaji wa kesi.

## MKALIMANI WA MAHAKAMA HAWEZI

- Kukupa ushauri wa kisheria au wa kibinafsi.
- Jibu maswali kuhusu sheria au mchakato wa kisheria.
- Kuzungumza nawe juu ya kesi yako.
- Eleza maana ya maneno, au kinachoendelea mahakamani.
- Kuwa na mazungumzo na wewe, familia yako, au mtu yeyote anayehusika katika kesi yako.

## TAARIFA MUHIMU

- Hakikisha unasoma na unaelewa barua zote kutoka kwa korti.
- Zingatia sana tarehe za usikilizwaji wa kesi na muda wa mwisho.
- Usipuuze wito, mashauri, au majukumu mengine ya kisheria.
- Fika kwa wakati kwa usikilizaji wa kesi yako
- Hakikisha anwani na mawasiliano yako (nambari ya simu, anwani ya barua-pepe) ambayo korti inavyo ni sahihi.
- Ikiwa unahitaji huduma za tafsiri au nafasi maalum kwa kuendesha kesi yako, omba msaada kwa kupiga simu **(520) 724-3888** mara tu unapojua tarehe na muda kesi itakavoendelea.
- Kwa taarifa kuhusu ada na gharama za kufaili, pamoja na kuondolewa ada na gharama, wasiliana na Karani wa Mahakama kwa **(520) 724-3200**.

